

Tarehe 05.04.2024

**TANGAZO LA ZABUNI YA USOMBAJI WA KAHAWA KUTOKA KWENYE MAGHALA YA
VYAMA VYA MSINGI HADI KEMONDO/KIWANDANI MSIMU 2024/2025**

Zabuni na: KCU/Z/2024/2025/09

1. KCU (1990) LTD Inamiliki inakaribisha zabuni ya magari makubwa (Malori) kwa ajili ya kusomba kahawa kutoka Vyama vya msingi kwenda Kwenda ghala la Kemondo/Kiwandani kwa msimu 2024/2025.
 2. Magari ni yale yaliyofunikwa sehemu yote ya kubeba mizigo (Box Board Truck) na yaliyo wazi lazima yawe na turubali imara.
 3. Mwombaji ataje bei zinazozingatia bei elekezi za EWURA.
 4. Mwombaji sharti ataje kwa kila gari; aina ya gari, uwezo wake wa kubeba mzigo.
 5. Mwombaji awe na leseni ya biashara pamoja na TIN/VAT na SUMATRA.
 6. Mwombaji sharti ataje bei kwa tani kwa kilometa ya kusafirisha kahawa kutoka vyama vya ushirika vya msingi hadi Kemondo/kiwandani.
 7. Mwombaji aeleze usalama wa mzigo utakavokuwa wakati akisafirisha kahawa hadi Tanga/Dar es salaam.
 8. Mwombaji aeleze uzoefu wa kazi alizowahi kufanya.
 9. Mwombaji aorodheshe namba za magari yatakayohusika na usombaji/usafirishaji wa kahawa.
 21. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 100,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955001 KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LTD** iliyopo CRDB
 10. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 1-10 vilivyo tajwa hapo juu.
 11. Barua za maombi zilizofungwa katika bahasha yenye lakiri na kuandikwa juu yake:-
"MAOMBI YA ZABUNI YA USOMBAJI WA KAHAWA KUTOKA KWENYE MAGHALA YA VYAMA VYA MSINGI HADI KEMONDO/KIWANDANI MSIMU 2024/2025" kwa anuani tajwa hapa chini,
- MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
12. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika ofisi ya manunuzi KCU (1990) Ltd kabla au mnamo tarehe 19.04.2024. saa 4.00 asubuhi siku ya Ijumaa na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni
 13. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.
Imetolewa na;

MENEJA MKUU
KCU (1990) LTD

